East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 4, Issue 1, 2019
ISSN: 1476-4687

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# UCHANGANUZI WA ATHARI YA MAGEUZI YA MANENO KWENYE MUUNDO WA SENTENSI YA EKEGUSII

*Wilfrida Kemuma Momanyi*[1], *Dkt. Beverlyne Asiko Ambuyo*[2] *& Prof. Rocha Mzungu Chimerah*[3]

[1]Chuo Kikuu cha Mount Kenya,, SLP 411 – 40200, Kisii, Kenya, winniekemuma@gmail.com.
[2]Chuo Kikuu cha Maseno, SLP 3275 – 40100, Kisumu, Kenya, bevambuyo@gmail.com.
[3]Chuo Kikuu cha Pwani, SLP 195 – 80108, Kilifi, Kenya, rocha.chimerah@yahoo.com.

**Article history:**

*Received: 24 Aug 2019*
*Accepted: 06 Sep 2019*
*Published: 06 Sep 2019*

**Keywords**:

*Dhima,*
*Fundo,*
*Mageuzi,*
*Ugeuzi,*
*Uhamisho,*
*Utegemezi Muundo,*
*Vigezo,*
*Ekegusii*

**IKISIRI**

Tasnifu hii inachanganua athari ya mageuzi ya maneno kwenye muundo wa sentensi sahili ya Ekegusii ikiangazia sheria na kanuni zinazotawala mageuzi hayo. Mageuzi ya kisintaksia huleta mabadiliko mengi katika sentensi asili. Utafiti huu ulichunguza na kuchanganua athari ya haya mageuzi kwenye muundo wa sentensi. Utafiti huu vilevile ulishughulikia viambajengo vya sentensi sahili ya Ekegusii kwa kudhihirisha kanuni mahususi zinazotawala muundo wa sentensi hiyo. Misingi ya kinadharia ya utafiti huu ni Sintaksia Finyizi kwa mujibu wa Chomsky. Data ilikusanywa maktabani kupitia kwa vitabu teule vya Ekegusii kwa kutumia kifaa cha kudondoa data. Mbinu ya usampulishaji kwa lengo maalum ilitumiwa ili kupata sentensi zilizodhihirisha mageuzi. Mbinu za maelezo zilitumika katika kuwasilisha data. Vijenzi vya sentensi sahili ya Ekegusii na dhana ya ugeuzi yanashughulikiwa ambapo majopo leksika na majopo amilifu yamejadiliwa kwa kina. Dhana ya ugeuzi na aina za mageuzi zinazojitokeza katika sentensi sahili ya Ekegusii pia imeshughulikiwa. Matokeo ya utafiti yanadhihirisha kwamba mageuzi yanayofanyiwa muundo wa sentensi hayabadilishi maana ya sentensi asili. Matokeo na mahitimisho ya utafiti wetu yanadhihirisha kwamba, suala muhimu linalojitokeza ni kuwa kanuni geuzi zinasababisha mabadiliko katika muundo wa sentensi ingawa maana ya sentensi hubaki ile ile. Pili ni kuwa mageuzi hayafanyiki kiholela; hufuata utaratibu unaokubalika na kutawaliwa na kanuni mahususi. Mwisho ni kuwa utafiti huu unapendekeza kuwa dhana ya mageuzi ya kisintaksia ishughulikiwe katika lugha nyinginezo kwa kurejelea sentensi ambatano na kwa nadharia nyinginezo za kisasa. Utafiti huu utawafaidi waundaji wa mitaala katika lugha ya Ekegusii. Vile vile, utafiti huu utaweka msingi bora katika eneo la isimu linganishi miongoni mwa watafiti wengine mbali na wale watakaoitafitia mada hii katika lugha nyinginezo. Matokeo ya utafiti huu yatachangia katika kuelewa zaidi ubainishi wa miundo mbalimbali ya sentensi za kibantu na kuwafaidi walimu katika ufunzaji wa sintaksia ya kibantu na hasa katika lugha ya Ekegusii.

## UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Thiong'o (1986), kuna uhusiano mkubwa kati ya lugha na maendeleo ya wanajamii watumizi lugha. Maendeleo haya hutokana na maelewano katika mawasiliano. Kuelewa maumbo ya maneno katika lugha na misingi ya maumbo hayo huchangia zaidi kuelewa lugha hiyo na kufanikisha mawasiliano na maelewano miongoni mwa wazungumzaji wa lugha husika. Kwa mfano, uhamishaji wa maumbo katika sentensi husababisha athari katika sentensi hiyo. Lugha za kienyeji husheheni tamaduni na amali za jamii husika. Kulingana na Thiong'o (1986), mtu ni utamaduni wake na lugha. Ili kumwelewa mtu barabara, inabidi basi kuifahamu sintaksia ya lugha yake. Waafrika wataeleweka zaidi wanapozitumia lugha zao za kienyeji.

Lugha ya Ekegusii ni lugha ya asili ambayo hubeba utamaduni wa Omogusii. Wazo hili lilimpa mtafiti msingi wa kufanya utafiti jinsi sentensi sahili ya lugha hii nia kuu ikiwa kuelewa zaidi miundo yake. Mawazo haya ya Thiong'o yalimsaidia mtafiti kufafanua umuhimu wa kuzingatia lugha ya Ekegusii kama sehemu muhimu ya kufafanua sarufi yake, hasa ikizingatiwa kuwa madhumuni makuu ya lugha yoyote ile ni mawasiliano. Utafiti huu ulichanganua mageuzi yanayofanyika katika sentensi baada ya kusogeza au kuhamisha viambajengo vyake kutoka pahali pao pa awali hadi pahali papya. Vile vile utafiti huu ulichunguza vikwazo vinavyotawala mageuzi ya sentensi za Ekegusii pamoja na mabadiliko ya kimuundo yanayoathiri sentensi husika. Misingi ya nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni ile ya Sintaksia Finyizi iliyoasisiwa na Noam Chomsky (1993, 1995). Kwa mujibu wa Chomsky, sarufi bia huandamana na ubia wa sarufi wa lugha zote za ulimwengu.

Kwa mujibu wa Mbaabu (1992), kila lugha ina upekee wa muundo na mpangilio wa maneno katika sentensi zake. Kazi za Guthrie (1948, 1971) na Nurse (1985) zinaonyesha kwamba barani Afrika mna makundi manne ya lugha nayo ni: *Niger Kordofanian, Nile Saharan, Afro-Asiatic* na *Khoisan*. Lugha za Kibantu ni miongoni mwa lugha katika kundi la *Niger-Kordofanian.* Lugha za Ekegusii na Kiswahili miongoni mwa zingine ziliainishwa kama lugha za nasaba moja. Muundo wa sentensi wa lugha za nasaba moja kama zilivyo Kiswahili na Ekegusii huonekana kufanana. Sifa moja kuu inayoitambulisha lugha za Kibantu ni kwamba nomino zake hupangwa kwenye makundi yanayoitwa ngeli na ambayo katika sentensi huonyesha upatanifu wa kisarufi. Lugha ya Ekegusii ni mojawapo ya lugha za kibantu zinazozungumzwa magharibi mwa nchi ya Kenya. Uasili wa uzungumzaji wa lugha hii nchini Kenya upo katika kaunti za Kisii na Nyamira. Guthrie (1948) ameianisha lugha ya Ekegusii kama lugha ya Kibantu ya kati ambayo inakaribiana na lugha zingine za kibantu zinazozungumzwa nchini Kenya na Tanzania. Lugha hizi ni Luloogoli, Kikuria, Kisuba na Kimeru za Kenya; vile vile Ware, Ikisu, Ikoma na Sanjo za Tanzania.

Jamii ya wazungumzaji wa lugha hizi huitwa Abagusii. Jamii ya Abagusii imezingirwa na jamii nyinine ambazo zinazungumza lugha tofauti nao. Jamii hizo ni za Kinailoti. Katika upande wake wa magharibi, Abagusii wamepakana na Wajaluo. Kwa upande wa kaskazini wamepakana na jamii ya Wakipsigis huku majirani zao upande wa kusini ni Wamaasai. Kwa mujibu wa wanahistoria, chimbuko la kundi la Abagusii ni eneo liloko kati ya Nigeria mashariki na Cameroon (Kapiyo na wenzake, 1996). Baadaye kulingana na wanahistoria hawa, jamii ya Abagusii ilihamia Congo kabla ya kuingia nchini Kenya kutoka upande wa magharibi na kuweka makao yao katika Milima ya Gusii. Hii, kulingana na sensa hiyo ni asilimia kumi ya jumla ya watu katika taifa la Kenya. Wengi wa watu hawa wanaishi mashambani ikilinganishwa na maeneo mengine.

Dhana ya ugeuzi imeshughulikiwa na wataalamu wengi wa lugha. Massamba (2004), amefafanua dhana ya ugeuzi kuwa ni utaratibu utumiwao kubadili umbo la tungo na kuwa umbo jingine kwa kutumia kanuni fulani maalum ambazo huitwa kanuni geuzi. Kwa mujibu wa Chomsky (1957, 1965), uchambuzi wa ugeuzi hujikita katika dhana kuwa baadhi ya tungo katika lugha huwa ni tungo msingi ilhali tungo ingine ni tokeo la mchakato wa uzalishwaji kutoka kwa hizo za msingi kupitia kanuni geuzi. Kwa mujibu wa Chomsky (1965), kuna mageuzi ya aina nyingi. Katika ugeuzi tunapaswa kujua jina la mageuzi, maelezo ya muundo wa sentensi na mabadiliko yanayotokea. Mabadiliko yatokeayo kufuatia mchakato wa

ugeuzi ni kama vile udondoshaji, uchopekaji na upanguaji wa vipashio kwenye sentensi. Maelezo haya yanapeana mwanga kuhusu dhana ya mageuzi kwa jumla na kuwa msingi kwetu katika kutalii mageuzi katika lugha ya Ekegusii.

Mageuzi hutawaliwa na kanuni maalumu kulingana na nguzo za Sarufi Bia. Chomsky (1965) anaeleza kuwa kanuni za sehemu msingi huzalisha seti iliyofinywa na mikufu msingi. Mikufu hii ina jukumu la ufafanuzi wa kimuundo unaoitwa kielelezo tungo msingi. Kielelezo tungo huzalisha umbo ndani la sentensi. Huu muundo ndani huelekea kwa kitengo geuza maumbo. Kitengo geuza maumbo hutekeleza mageuzi kama vile kudondoa na kuondoa, kuchopeka, ugeuza maswali, usogeziau, uhamishaji wa vipashio na kadhalika. Kitengo geuza maumbo kina aina kadha ya vikwazo vinavyoathiri mageuzi. Radford (1997) anaeleza kuwa sharti la ukaribu linadai kuwa hakuna kiambajengo kinaweza kuhamishwa zaidi ya fundo funge mbili katika utekelezaji wa kanuni yoyote. Kulingana na kanuni za nadharia ya Sarufi Bia, utafiti huu unachunguza ikiwa kanuni hii inaafikiana na zile kanuni zinazotawala mageuzi katika lugha ya Ekegusii.

Nadharia ya Sintaksia Finyizi ya Chomsky (1995) ina mashikilio kuwa lugha za ulimwengu huandamana na ubia wa sarufi. Utafiti huu unachanganua mageuzi ya kisintaksia katika lugha ya Ekegusii kama kigezo mojawapo cha ubia wa sarufi. Zaidi ni kuwa nadharia nyingi zimetumiwa kuchanganua Sintaksia. SF kama Sarufi Bia inaendeleza imani kuwa sintaksia ni kitengo msingi zaidi cha muundo wa kisarufi. Katika kuangalia sentensi, SF inatambua hatua tatu muhimu: idadishi ya maneno kupitia majopo ya kisarufi, muungano wa maumbo ili kuunda sentensi sanifu na uhamisho wa maumbo katika kugeuza muundo wa sentensi. Mbali na hizi hatua, SF vile vile ina vikwazo ambavyo huzingatiwa, navyo ni: uhamisho hutekelezwa tu pale ambapo unakubalika wakati na mahala ambapo panafaa, uhamisho hutekelezwa pale ambapo kihamisho huafiki na hujitosheleza kimofolojia, na uhamisho hutekelezwa tu kwa kuzingatia hatua chache. Utafiti ulinuia kuchunguza kama mageuzi ya sentensi za Ekegusiii yaliafikiana na hizi hatua na hivi vikwazo vya SF katika uundaji na uchanganuzi wa sentensi zake.

Kulingana na misingi anuwai iliyowekwa na wataalam kuhusu sarufi, kila lugha ina vikwazo na kanuni zinazofuatwa katika matumizi yake. Baadhi ya kanuni hizi zimeelezwa kuwa bia na husababisha kuwepo kwa miundo mbalimbali ya sentensi katika lugha mbalimbali. Suala la ugeuzaji wa maumbo ya maneno ni msingi mojawapo ambao huathiri miundo ya sentensi. Hivyo basi utafiti huu unanuia kuchanganua mageuzi ya maneno katika sentensi sahili ya Ekegusii na kubainisha kanuni zinazotawala mageuzi hayo. Kwa misingi ya tafiti za awali katika lugha nyinginezo, utafiti huu unajaza pengo la kufafanua mageuzi ya maneno katika sentensi sahili ya Ekegusii kama msingi muhimu wa kuelezea sarufi ya lugha hii.

## MALENGO YA UTAFITI

Katika kuangazia mada hii ya mageuzi ya maneno kuathiri muundo wa sentensi, utafiti huu ulinuia kuafiki malengo yafuatayo: kubainisha kanuni na sheria zinazotawala muundo wa maneno katika sentensi sahili ya Ekegusii; kuchanganua aina za mageuzi katika maneno ya sentensi sahili ya Ekegusii; kupambanua kanuni zinazotawala mageuzi katika sentensi sahili ya Ekegusii na kutathmini athari za mageuzi kwa maneno ya sentensi sahili ya Ekegusii.

## MISINGI YA UTEUZI WA MADA

Watafiti walichochewa kutafitia mada hii kwa sababu ya umuhimu kuzielewa luhga za kienyeji na hasa lugha ya Ekegusii ambayo ina wazungumzaji takriban milioni mbili nukta mbili kulingana na sensa ya 2009. Lugha za kienyeji husheheni tamadunina amali za watumizi lugha wake. Lugha hizi huwa ni kigezo cha maendeleo yake na kwa hivyo kwa kuzitafitia,mtafiti atakuwa amechangia katika maendeleo ya jamii hii mbali na kuchangia pia katika taaluma ya isimu ya lugha ya Ekegusii. Uchaguzi wa mada ya uchanganuzi wa athari za mageuzi ya maneno kwenye muundo wa sentensi sahili ya Ekegusii ulitokana na matarajio kwamba matokeo ya utafiti huu yana nafasi ya kutoa mchango wa kinadharia katika taaluma ya isimu, kwa kutumia nadharia zilizopo kwa mfano ile ya Chomsky (1965) ya ubia wa sarufi. Ubia wa lugha unahusu mambo kadha ambayo yalichochea uteuzi wa mada hii. Baadhi ya mambo hayo ni sifa ya kuwa na ufafanuzi toshelevu, uasilia wa lugha

inayochunguzwa, upekee wa lugha ya mwanadamu na utumiaji wa vipengee vichache vyenye utoshelevu. Ubia wa lugha kwa mtazamo wa Chomsky unajikita katika imani kuwa kunayo idadi maalum ya sheria ambazo hufanya kazi kwa lugha zote za ulimwengu huu. Utafiti huu ulinuia kuziweka wazi hizi sheria katika lugha ya Ekegusii. Mada hii kwa hivyo inaendeleza na kuchangia ubia wa lugha ya Ekegusii.

## NADHARIA YA UTAFITI

Nadharia tofauti zimetumika kuchanganua sintaksia kwa mfano ile ya Sarufi Zalishi iliyoendelezwa na Chomsky (1957, 1965, 1981, 1986 na 1993). Malengo ya Chomsky yalikuwa kuweka misingi ya kanuni za kijumla za Sarufi Bia za lugha ya binadamu. Alisisitiza vigezo vya kisintaksia kama nanga muhimu ya sarufi. Nadharia ya Sarufi Zalishi ilipitia hatua mbalimbali kama vile kubainisha dhana ya umilisi na utendaji wa lugha pamoja na kutenganisha miundo ya sentensi katika sehemu mbili: muundo ndani na muundo nje. Mbali na haya, mtazamo huu ulibainisha aina mbili za kisintaksia: sheria mageuzi na sheria msingi. Mitazamo hii iliendelezwa zaidi na kuelezwa zaidi katika Sintaksia Zalishi Pambanuzi na Chomsky (1981-1990). Katika kazi hii Chomsky alifafanua kanuni bia na vigezo bayana vinavyohitaji kuendeleza Sarufi Bia ya Isimu Zalishi. Vigezo ni zile hali bayana zaidi ambazo zaweza kutofautisha lugha moja na nyingine. Nadharia hii ya sarufi zalishi ilifaa katika utafiti huu hasa katika kubainisha miundo ya sentensi katika sentensi sahili ya Ekegusii. Mtazamo wa Utawala na Ufungami ulijumuisha vijinadharia sita: X-baa, utawala, uhusika, dhima maana, ufungami na ufundani. Mbali na vijinadharia hivi sita, mtazamo wa Utawala na Ufungami ulitambua viwango viwili vya muundo wa sentensi: Muundo wa ndani na muundo wa nje.

## UHAKIKI WA MAANDISHI

### Sheria Zinazotawala Muundo wa Maneno Kisintaksia

Kwa mujibu wa Kamusi ya Karne 21 Lorghorn (2011), sintaksia ni tawi la isimu linaloshughulikia uchanganuzi, mpangilio na uhusiano wa vipashio katika sentensi. Kwa mujibu wa Kapinga (1983), sintaksia ni mojawapo ya ngazi za isimu iliyo kati ya mofolojia na semantiki na huchunguza muundo wa sentensi ya lugha na viambajengo vyake kama vile mofu, maneno, virai na vishazi. Vipashio hivi vina uhusiano mkubwa na huungana katika kuunda kipashio kinachoitwa sentensi. Taaluma hii inahakiki namna maneno yanavyopangwa ili kuunda tungo na sentensi zenye maana katika lugha. Hivi ni kumaanisha kwamba sentensi si kitu kilichopangwa kiholela bali ni mpangilio wa kidaraja unaofuata utaratibu maalum. Utafiti huu kwa hivyo ulinuia kubainisha hizo kanuni na sheria zinazotawala muundo wa maneno katika sentensi sahili ya Ekegusii ili kubainishawazi utaratibu huo.

Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004), kitengo cha sintaksia kina vijitengo viwili. Kwanza kuna kijitengo msingi na pili kuna kijitengo geuzi. Fasirihizi zilimpa mtafiti mwongozo wa kiwango cha isimu ambacho kilishughulikiwa mbali na kumpa msingi bora wa kufanyia utafiti. Pili ni kuwa fasiri hizi ziliainisha mwongozo wa mpangilio wa maneno katika sentensi ya Ekegusii na kuchunguza ikiwa mpangilio huu ungeafikiana na ile mipangilio ya Kiingereza iliyozungumziwa na hawa waandishi. Kulingana na Bornstein (1978), sheria za miundo virai ni sheria zinazoonyesha kuandikwa tena kwa viambajengo. Hizi sheria ambazo zinaweza kuzalisha sentensi katika lugha huitwa sheria miundo virai.

Viambajengo hivi huunganishwa kwa kufuata kanuni fulani. Taaluma ya sintaksia huchunguza kitengo mbalimbali za maneno kulingana na utendakazi wake katika sentensi. Kategoria hizi ni nomino, viwakilishi, vitenzi, vihusishi, vielezi, viunganishi, vivumishi na vihisishi; Hizi ndizo kategoria ambazo hutumiwa katika sentensi. Kategoria hizi ndizo hutumika katika uundaji wa maneno. Kunazo sheria ambazo hufuatwa katika uundaji wa sentensi, kwa mfano, sentensi ya Kiswahili hufuata muundo wa NVTE (Nomino + kivumishi + kitenzi + kielezi) (Poole, 2002).

Kwa mujibu wa Chomsky (1986), kwa mfano, nadharia geuzi ina vitengo vitatu: Fonolojia, sintaksia na semantiki. Kitengo cha sintaksia hushughulikia uundaji wa sentensi. Kitengo hiki ni muhimu katika kazi yetu kwani ndicho kinachoshirikisha sauti za lugha na maana kupitia miundo mbalimbali ya kisintaksia. Aidha, kijitengo

geuzi ndicho kinachogeuza sentensi kutoka muundo wa ndani hadi wa nje. Utafiti huu ulinufaika pakubwa na mchango wa wanaisimu hawa. Kijitengo geuzi huhusisha kauli mbili kwa mujibu wa utafiti huu: Kauli tenda na kauli tendwa. Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (1999), lugha za kibantu hushabihiana kimuundo na kisifa. Aidha, wanaongezea kuwa lugha hizo huwa na mfuatano wa viambishi na mizizi. Viambishi katika lugha hizi huweza kutokea mwanzoni au baada ya mizizi. Baadhi ya sentensi za lugha ya Ekegusii zina sifa mahususi kwa maana kwamba miundo ya sentensi hizo inatofautiana sana na miundo ya lugha za Kinailoti kwa mfano, ambao wamepakana nao, au zile za Ulaya ambazo kwa kiasi kikubwa ndizo zimetumiwa kubuni kanuni za sasa za uchanganuzi wa sentensi.

**Mageuzi ya Maneno**

Mageuzi ya maneno katika sentensi huathiriwa na kauli kwani hatuwezi kuzungumzia mageuzi bila kushughulikia dhana ya kauli. Masamba na wenzake (1999) wanena kuwa dhana ya kauli katika sarufi kuhusu uhusiano uliopo baina ya ama kitenzi na kiima au kitenzi, kiima na yambwa. Kwa ufupi dhana hii inahusu mtenda na mtendwa katika sentensi. Kagwa na wenzake (2013) wameigawa dhana ya kauli katika aina kuu mbili ambazo ni kauli ya kutenda na kauli ya kutendwa. Kauli ya kutenda hudhihirisha kwamba kiima katika sentensi inayohusika ina uamilifu wa kutenda jambo. Katika sentensi tenda yambwa huathirika kwa namna fulani. Kuathirika huku ni kwa namna ya kufanyiwa mageuzi ambapo viambajengo hudondoshwa, huchopekwa, ilhali vingine vikihamishwa.

Kauli ya kutendewa inaashiria kuwa kiima kina uamilifu wa kutendwa, yaani kiima kinafanyiwa tendo fulani. Sentensi tenda na tendwa zinahusiana pakubwa. Uhusiano huu unajitokeza baina ya kiima, kitenzi na yambwa katika makundi yote mawili ya sentensi. Kitenzi kinaonekana kuwa kiini cha uhusiano huo kwa sababu kinahusisha mtenda na mtendwa. Tofauti zilizoko ni za kimuundo tu. Katika sentensi tenda, kiima kinachukua uamilifu wa mtenda na yambwa inachukua uamilifu wa mtendwa. Kwa hivyo mageuzi hutokea katika kauli ya tendwa.

Dhana ya kauli ni muhimu katika utafiti huu kwani iliwezesha kubaini ni mambo yapi hufanyikia sentensi katika hali ya mageuzi. Dhana hii ilisaidia kubaini pia ni viambajengo gani huingizwa katika sentensi za kauli mbalimbali na ni zipi huondoshwa mbali na kuwezesha kutambua vile viambishi vinavyopachikwa katika kauli mbalimbali.Utafiti ulijikita katika kauli hizi mbili kwani ndizo zinazopatikana sana sana katika sentensi sahili ambayo ndiyo eneo la utafiti wetu. Kauli zingine kama vile za kurejelea, kutendana, kutendeka na kadhalika haziingiliani sana na eneo la utafiti huu. Katika kubainisha dhana ya kauli, utafiti huu ulibidi vilevile uangalie dhana ya sarufi geuzi na sarufi zalishi.

Sentensi ni kipashio kikubwa cha kimuundo chenye maana kamili (Massamba na wengine, 1999). Miundo ya sentensi uhusisha vipashio vingine vidogo kimiundo. Vipashio hivyo ni virai na vishazi. Kazi ya waandishi hawa imekuwa na mashiko makubwa katika utafiti wetu kwa sababu viambajengo vya sentensi vilivyotajwa na wataalamu ndivyo vimekuwa nguzo za utafiti wetu kwa jumla. Mbali na hayo imetufaa katika kazi hii kwa sababu imetuwezesha kubaini viambajengo vya sentensi. Hali kadhalika kazi yao imerahisisha utafiti huu kwa jumla na pia kuangazia viambishi vinavyopachikwa kwenye mzizi wa neno mbali na kushughulikia dhana ya upatanishi wa kisarufi katika sentensi. Sifa hizi mahsusi zinazojadiliwa zina umuhimu wake katika dhana ya uchanganuzi wa sentensi sahihi ya Ekegusii

**Kanuni Zinazotawala Mageuzi Katika Sentensi**

Sarufi Geuzi ni utaratibu wa kubadili maumbo ya maneno kuwa maumbo mengine kwa kufuata kanuni maalum. Sarufi hii hujengwa kwa wazo kwamba katika lugha kuna sentensi ambazo huwa ni za msingi ambazo hutokana na kaida mahsusi.Sentensi zingine huweza kuzalishwa na sentensi hizo (Matinde, 2012). Ugeuzaji ni mbinu ya kisarufi ambayo hutumiwa katika sarufi geuzi maumbo zalishi kuzalisha sentensi nyingi kwa kufuata sheria na kanuni maalum. Matokeo ya mageuzi haya ni uchopekaji wa viambajengo, udondoshaji wa vingine na uhamishaji wa maumbo ambao huathiri mpangilio wa maneno katika sentensi. Utafitu huu ulinuia kuchanganua aina za mageuzi katika sentensi sahili ya Ekegusii,

kupambanua kanuni zinazotawala mageuzi hayo na kutathmini athari za mageuzi hayo.

Kulingana na kanuni za nadharia ya Sarufi Bia ya Chomsky (1993), kila lugha ina vikwazo na kanuni zinazofuatwa katika matumizi yake. Utafiti huu unachunguza dhana ya mageuzi katika sentensi za Ekegusii ili kubainisha ikiwa yanaafikiana na hizi sheria za Sarufi Bia. Mageuzi huleta athari nyingi katika sentensi asili. Athari au mifanyiko hii huchunguzwa ili kujua inatawaliwa na nini. Ingawa watafiti kama vile Kawa (2003) wameshughulikia suala la uhamisho wa kisintaksia suala la mageuzi ya maneno katika sentensi ya Ekegusii halikuwa suala lao la utafiti. Kwa mfano, Kawa (2003) alishughulikia uhamisho wa kundi nomino katika sentensi ya Kiswahili. Isitoshe hawa hawakujishughulisha na athari kwa muundo wa sentensi baada ya hayo mageuzi. King'ori (2005) alishughulikia uhamisho wa kichwa na kikanushi katika sentensi. Hivyo basi ni wazi kwamba mageuzi ya kisintaksia na athari zake katika muundo wa sentensi ni suala ambalo lilifaa kuchunguzwa ili kurotubisha mada hii ya mageuzi. Isitoshe kati ya wale walioshughulikia mada hii wamefanya hivyo katika lugha za Kiswahili, Kiembu, na Kibukusu.

Muundo wa sentensi wa lugha ya Ekegusii kwa hivyo ni eneo ambalo lilifaa kushughulikiwa hasa ikikumbukwa kwamba kila lugha ina upekee wake kimuundo. Mbali na tafiti nyinginezo zilizofanywa kama vile ya Ambuyo (2007) aliyeshughulikia uamilishi dhima katika sentensi za Lulogooli, utafiti huu ulishughulikia mageuzi katika sentensi ya Ekegusii. Hata hivyo kazi hii ilinufaika kutoka kwake kwa sababu Ekegusii na Luloogoli ni lugha za Kibantu za nasaba moja. Isitoshe, wengi ambao wametafitia sintaksia ya lugha za Kiafrika wametumia nadharia nyinginezo huku utafiti wetu ukitumia nadharia ya Sintaksia Finyizi ili kujaza pengo hili.

Mageuzi yameainishwa kwa makundi mawili makuu yale ya shuruti na yale ya hiari. Omondi (1992) anaelezea ugeuzi kuwa 'utaratibu wa kisarufi ambao unapotekelezwa kwenye mfululizo wa ishara za kileksia katika mfumo fulani hutoa athari fulani'. Kijitengo geuzi ndicho kinachoonyesha jinsi ya kugeuza sentensi kutoka muundo mmoja hadi mwingine. Utafiti huu ulitupa mwanga wa jinsi ya kugeuza sentensi kutoka muundo mmoja hadi mwingine na athari ya mageuzi hayo katika muundo wa sentensi sahili ya Ekegusii.

**Tafiti Bayana za Kisintaksia za Lugha ya Ekegusii**

Kazi za kina zilizobainisha muundo wa lugha ya Ekegusii zimeeleza vijenzi pamoja na sifa mbalimbali za lugha hii. Kategoria za kisarufi pia zimeshughulikiwa kwa kiasi kikubwa kuzingatia chukulizi za sifa za lugha za Kibantu. Uainishaji wa lugha za Kibantu ulifanywa na Guthrie (1948). Lugha za Ekegusii na Kiswahili ziliainishwa kama lugha za Kibantu, Kiswahili kikiwekwa katika kundi la G na Ekegusii katika kundi la E. Kazi hii ni msingi bora kwetu katika kuitafitia sintaksia ya lugha ya Ekegusii kwani ilitupa msingi bora wa sifa za lugha hii ambao ulitusaidia katika kubainisha miundo ya sentensi za lugha hii na sheria na kanuni zinazotawala mpangilio wa maneno katika sentensi ya lugha hii.

Gesare (1992) alitafiti mofolojia ya Ekegusii ambapo alionyesha kuwa maneno katika lugha hii yanaweza kutenganishwa kwa vipashio vyake na kila kipashio kikawa na maana mahususi. Utafiti huu ulikuwa muhimu katika kutalii mofosintaksia katika lugha ya Ekegusii. Basweti (2005) alichunguza mofosintaksia ya nomino na elementi za sentensi za Ekegusii. Utafiti huo ulipania kuchunguza muundo wa kimofolojia na sintaksia.Otiso (2008) naye alichunguza vitenzi vya Ekegusii kwa kutumia nadharia ya Uminimalisti. Alionyesha kwamba katika mofolojia ya Ekegusii vitenzi huongezewa viambishi awali na tamati ili kuonyesha hali na njeo za vitenzi. Utafiti huu ulitufaa katika kurejelea mageuzi yanayofanyikia vitenzi vya Ekegusii baada ya uhamisho kutoka pahali pao pa awali katika sentensi hadi pahali papya.

Mayaka (2000) alichunguza na kujadili muundo wa sentensi katika lugha ya Ekegusii akitumia nadharia ya Sarufi Zalishi Geuza Maumbo. Alitazama sentensi sahili, ambatani na changamano kwa kuzingatia nadharia ya Sarufi Zalishi Geuza Maumbo ambapo alibainisha kuwa sentensi huundwa kwa kushirikisha viambajengo mbalimbali kwa kutumia utaratibu unaokubalika

lakini utafiti wetu umepiga hatua kwa kutumia nadharia ya Sintaksia Finyizi katika kuangalia zile kanuni za mageuzi katika sentensi ya Ekegusii. Ingawa kazi hii ni tofauti na ile iliyo tafitiwa, lakini ilitusaidia katika uchanganuzi wa sentensi sahili. Kazi hii ilitusaidia katika kutupa mwongozo bora wa muundo wa sentensi ya Ekegusii.

**Tafiti Zilizotumia Nadharia ya Sintaksia Finyizi na Sarufi Geuza Maumbo**

Nadharia ya Sintaksia Finyizi imetumiwa na watafiti si haba katika kazi zao huku ikionekana kuwaletea matokeo waliyotarajia. Kwa mfano, Ambuyo (2007) alishughulikia uamilishi dhima katika sentensi ya Luloogoli kwa mtazamo wa Sintaksia Finyizi. Utafiti wake ulijadili kuwa kitenzi kina nafasi kubwa katika uamilishi dhima wa maana ya nomino katika sentensi sahili ya Luloogoli. Tofauti naye utafiti huu ulishughulikia mageuzi ya kisintaksia katika sentensi ya Ekegusii kwa mtazamo wa SF huku tukitaka kutathmini ufaafu wake katika kazi hii.

Ombuna (2004) ametafitia valensi ya kitenzi katika kishazi cha Kiswahili huku uchanganuzi wake wa data ukijikita katika mihimili ya SF kwa madhumuni ya kubainisha muundo wa valensi ya kitenzi katika kishazi huru cha Kiswahili. Katika utafiti huu ilibainika kuwa kitenzi cha Kiswahili hudhihirisha muundo wa valensi ya dhima kapa, dhima moja, mbili na tatu. Kazi ya Ombuna ilikuwa mwongozo bora katika kushughulikia muundo wa sentensi sahili ya Ekegusii. Vilivile mpangilio wa maneno katika sentensi ulitoa mwongozo katika utaratibu wa kufuatwa katika kufanya mageuzi yanayokubalika katika sentensi.

Katika kazi ya Mose (2013), aliyeshughulikia muundo wa dhima ya kirai nomino katika sentensi ya Ekegusii, ufaafu wa SF kama nadharia ya utafiti imedhihirika na kumpa matokeo aliyotarajia. Wengine ni Otiso (2008) na Gesare (1992) waliotumia nadharia hii katika kazi zao. Kutokana na mifano hii michache ni kuwa nadharia ya Sintaksia Finyizi imetumika katika tafiti nyingi na watafiti wengi na kuleta matokeo bora na kwa hivyo utegemezi wake kama nadharia ya utafiti ni wa kutegemewa katika tafiti zilizofanywa. Utafiti huu ulikusudia kutathmini kama nadharia hii itafaa katika kazi hii.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Kwa mujibu wa Hendrick, Brickman na Debra (1993), lengo la utafiti wa kimaelezo ni kutoa picha mahususi ya kitafitiwa katika mazingira yake halisi na kupata picha ya hali ya jinsi vitu vinavyohusiana. Mugenda (2008) naye anakubaliana na Hendrick kwamba utafiti wa kimaelezo huweka msingi ambapo kitu kinaweza kuelezwa ili kutoa tofauti au sifa zingine zinazojitokeza. Utafiti huu umetoa maelezo ya athari ya mageuzi ya maneno kwenye muundo wa sentensi sahili ya Ekegusii. Data iliyotumika katika utafiti huu ilipatikana kutoka vitabu teule vya Ekegusii vilivyoidhinishwa na Wizara ya Elimu kwa ufunzaji wa wanafunzi wa shule ya msingi wa darasa la kwanza hadi la tatu. Muundo wa kimaelezo ulitoa maelezo ya kina ya mageuzi ya kisintaksia na athari zake katika muundo wa sentensi ya Ekegusii. Michoro matawi na mishale ilitumiwa kuwasilisha na kujadili data.

Eneo letu la utafiti ni sentensi sahili ya Ekegusii. Sentensi hizi ziliteuliwa kutoka vitabu teule vya Ekegusii vinavyotumika katika shule za msingi na vilivyoidhinishwa na Wizara ya Elimu. Idadi ya sentensi thelathini na saba (37) ziliteuliwa ikiwa ni theluthi moja ya jumla ya sentensi mia moja kumi na nne (14) zilizodondolewa kutoka kwa vitabu hivi. Sentensi sahili ilimfaa mtafiti kwani ndiyo sentensi msingi na mageuzi yote yanafanyika kutokana na sentensi sahili Chomsky (1995).

Kundi legwa katika utafiti huu ni sentensi sahili za Ekegusii. Sentensi hizi zilipatikana kutoka kwenye baadhi ya vitabu teule vya Ekegusii vilivyoidhinishwa na Wizara ya Elimu kutumika katika shule za msingi. Jumla ya vitabu vitano vya lugha ya Ekegusii vilitumika kati ya vitabu kumi na sita vilivyopatikana katika maktaba ya jamii.

Usampulisaji wa kimaksudi ulitumiwa. Mtafiti alisampuli sentensi hizi kwa kuzingatiasifa za sentensi sahili ambazo ni arifu, yakinishi na katika kauli tenda na tendwa. Sentensi sahili zilizofanyiwa mageuzi pia zilisampuliwa. Mtafiti alisampuli kiasi ya sentensi ambacho kiliafiki madhumni ya utafiti huu. Kwa mujibu wa Flick (2010), usampulishaji wa kimaksudi unaweza kutumika kuteua data ambayo itatimiza mahitaji ya mtafiti bila kuwa

haswa na idadi kamili ya data mradi tu mahitaji ya mtafiti yametimizwa.

Utafiti ulitumia uchunguzi wa matini kutoka kwenye baadhi ya vitabu teule vya Ekegusii vilivyoidhinishwa na Wizara ya Elimu kwa darasa la 1-3. Vitabu vilivyotumika ni pamoja na *Nyakundi n' Enyange yaye* (Baiskeli ya Nyakundi), *Etigere ya Ragira* (Punda wa Ragira), *Ekero gi' Echiro* (Siku ya Soko) na *Engoko ya Kerubo* (Kuku wa Kerubo). Sentensi zilizosheheni mageuzi ya kisintakisia ziliteuliwa. Kifaa cha kudondoa data kilitumika kukusanya data. Sentensi sahili za Ekegusii ziliteuliwa. Sentensi hizi zilikuwa arifu, yakinishi na katika kauli tenda na tendwa. Sentensi hizi zilidhihirisha dhima mbalimbali zinazoweza kuelezea kwa uwazi zaidi kanuni zinazotawala mageuzi ya maneno. Hii ilifanywa kwa kufanya majaribio ya mageuzi kwa kuzingatia kanuni zinazohitajika. Data ya maktabani ilipendelewa kwa sababu inadhihirisha ufasaha kwa matumizi ya lugha zaidi kuliko data ya nyanjani

Kifaa cha kudondoa data chenye sifa zinazotambulisha vipashio na miundo mbalimbali ya sentensi sahili ya Ekegusii kilitumika katika kukusanya data. Data iliyokusanywa ilisampuliwa kimakusudi. Data iliyotumika ilikusanywa kutoka maktaba ya jamii. Data yenyewe ni sentensi sahili za Ekegusii zilizotokana na orodha ya vitabu vinavyotumika kufunzia lugha ya Ekegusii. Wafiti waliteua idadi ya sentensi zilizotosheleza mahitaji ya utafiti huu kwani sentensi hizo zilisampuliwa kimaksudi. Vitabu vitumikavyo katika darasa 1-3 vilifaa utafiti huu kwa sababu ufunzaji wa lugha katika kiwango hicho ni wa kimsingi zaidi. Sentensi zilizopatikana katika vitabu hivyo kwa hivyo ni za kimsingi na vilevile sahihi kisarufi kwa sababu vitabu hivi vimeidhinishwa na Wizara ya Elimu. Sentensi ya kimsingi katika sintaksia ni sentensi sahili. Mageuzi yote yanayofanyika hutokana na sentensi sahili (Chomky, 1995).

Sentensi sahili ilifaa katika utafiti huu kwa sababu inabainisha mahusiano ya vipashio katika sentensi kwa vyema zaidi. Isitoshe sentensi sahili ina sifa ya kugawika kwa uwekevu zaidi hadi vipashio vidogo ili kubainisha zile kanuni na sheria zinazotawala muundo wa sentensi hiyo. Sentensi zilidondolewa kimaksudi kufikia kiwango ambacho kilitosheleza mahitaji ya utafiti. Kifaa cha kudondoa data kiliweza kutumika kudondoa idadi ya sentensi sahili zilizotosheleza madhumuni ya utafiti huu. Kifaa hiki kiliweza kudondoa sentensi zilizobainisha miundo mbalimbali, kuchanganua aina za mageuzi katika sentensi hizo, kupambanua kanuni zinazotawala mageuzi hayo na kutathmini athari za mageuzi kwa maneno ya sentensi hizo. Kifaa hiki kiliweza kutosheleza madhumuni ya utafiti huu.

Uchanganuzi wa data ulianza kwa kuainisha sentensi sahili za Ekegusii. Pili aina za mageuzi yanayofanyikia maneno katika sentensi hizo yaliainishwa. Athari za mageuzi hayo kwa muundo wa sentensi pia zilitathminiwa kwa kuzingatia nadharia ya Sintaksia Finyizi na ile ya Sarufi Geuza maumbo. Mtafiti alichanganua data kwa kusudi la kubainisha sheria na kanuni zinazotawala muundo wa sentensi sahili ya Ekegusii. Vilevile data ilichanganuliwa kwa lengo la kubainisha aina za mageuzi katika maneno ya sentensi hiyo.Kanuni zinazotawala mageuzi katika sentensi hizo zilipambanuliwa na hatimaye mtafiti alitathmini athari za mageuzi kwa maneno ya sentensi sahili ya Ekegusii. Maelezo, michoro matawi na mishale ni njia zilizotumika katika uchanganuzi wa data.

Mbinu za maelezo, michoro matawi na mishale zilitumika katika kuwasilisha data. Data iliwasilishwa kwa kuelezea miundo mbalimbali ya sentensi sahili ya Ekegusii. Maelezo ya kanuni zinazotawala mageuzi yalitolewa. Vile vile, maelezo ya aina mbali mbali za mageuzi yalitolewa. Mwisho ni kuwa athari za mageuzi haya katika sentensi ya Ekegusii yalielezwa. Maelezo haya yaliwasilishwa kwa njia ya michoro na matawi kuonyesha miundo iliyoundwa baada ya mageuzi.

## MATOKEO YA UTAFITI

Utafiti huu ulitekelezwa ili kuchanganua athari ya mageuzi ya maneno kwenye muundo wa sentensi ya Ekegusii. Lengo la utafiti lilikuwa kubainisha aina ya mageuzi yanayofanyikia maneno ya sentensi sahili ya Ekegusii, kanuni zinazotawala mageuzi hayo na athari ya mageuzi hayo kwenye muundo wa sentensi sahili ya Ekegusii. Mageuzi yaliyoshughulikiwa hapa ni geuzi tendwi na geuzi hamishi. Nadharia ya Sintaksia Finyizi kama sarufi bia inaendeleza imani kuwa sintaksia ni kitengo

msingi zaidi cha muundo wa kisarufi. Katika kuangalia sentensi, sarufi inatambua hatua tatu muhimu:

i. Idadishi ya maneno kupitia majopo ya kisarufi.
ii. Muungano wa maumbo ili kuunda sentensi sanifu.
iii. Uhamisho wa maumbo katika kugeuza muundo wa sentensi.

Sarufi inatawaliwa na kanuni sita muhimu ambazo zilituongoza katika kutekeleza malengo yetu katika uchunguzi huu. Kanuni hizi ni:

a) Kanuni ya utegemezi muundo.
b) Kanuni ya utawala.
c) Kanuni ya uhusika.
d) Kanuni ya ufasiri kamili.
e) Kanuni ya ufungami
f) Kanuni ya uarifu.

Sentensi za Ekegusii ziliteuliwa kutoka vitabu vya Ekegusii vilivyoidhinishwa na Wizara ya Elimu. Sentensi zilizoteuliwa ni zile tendwi na hamishi ambazo zilisheheni mageuzi katika muundo wao na pia zile tendi ambazo ziIifanyiwa majaribio ili kuona namna ambayo mageuzi hutokea na athari ya mageuzi hayo katika sentensi hizo. Muundo wa sentensi sahili ya Ekegusii pia ulishughulikiwa kwa kina.

Utafiti huu pia ulielezea viambajengo vya sentensi za Ekegusii, dhima zinazojitokeza na mageuzi katika sentensi hizo. Mabadiliko ya kimuundo yanaonyesha kwamba geuzi tendwi na geuzi hamishi hutegemea sana kiarifu, kiima na shamirisho/yambwa. Katika sura hii, muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo ya utafiti yatashughulikiwa. Utafiti huu umeshughulikia viambajengo vya sentensi sahili ya Ekegusii kwa kudhihirisha kanuni mahsusi zinazotawala muundo wa sentensi hiyo. Muundo wa kisintaksia wa sentensi hizi umeongozwa na kanuni bia na vigezo vinavyohitajika kuendeleza sarufi bia ya isimu zalishi. Kanuni hizi bia ni pamoja na utegemezi muundo, ufungami, kanuni leksia, ufasiri kamili, ufundani na upatanisho wa kisarufi.

Uchanganuzi wa sentensi za Ekegusii umedhihirisha kuwa sentensi hizo huundwa kutokana na majopo ya maneno kisarufi. Majopo hayo ni leksia na amilifu. Majopo leksia huhusisha maneno kama vile nomino, kivumishi, kitenzi, kielezi, vihusishi pamoja na virai vyao. Nayo majopo amilifu huhusisha vibainishi, viunganishi na shamirisho au yambwa. Muundo wa virai vya Ekegusii vile vile umejadiliwa. Virai vya Ekegusii vimedhihirika kuundwa kutokana na maneno leksia. Katika kuunda kirai, imedhihirika kuwa maneno hayo huungana na lile neno tawala likawa ndilo linaunda kirai husika. Utafiti wetu ulipata virai leksia vitano ambavyo ni: kirai nomino, virai vivumishi, virai vitenzi, virai vihusishi na virai vielezi. Virai amilifu navyo ni vitatu kutokana na matokeo ya utafiti huu: virai viunganishi, virai vibainishi na virai shamirisho. Hizi aina mbili za virai leksia na amilifu huungana ili kuunda virai vikubwa zaidi ambavyo ni sentensi. Majopo ya maneno ni lazima yahusiane vizuri kwa kufuata sheria za uudaji wa sentensi ili kuunda sentensi sahihi. Miundo ya sentensi hutegemea virai vilivyotumiwa katika kuziunda. Sentensi iliyoshughulikiwa katika utafiti huu ni sentensi sahili. Dhana ya ugeuzaji wa maumbo imeelezwa na kudhihirishwa namna inavyotokea kwa kutumia mistari na michoro matawi. Imedhihirika kwamba katika ugeuzi umbo la sentensi hubadilika ili kuwa tofauti lakini maana hubakia ile ya msingi baina ya maumbo hayo tofauti.

Ilibainika kuwa sentensi ya Ekegusii inaweza kudhihirisha hali mbili: kwanza, muundo wa sentensi kabla ya kufanyiwa mageuzi na pili, baada ya kufanyiwa mageuzi sentensi inapata umbo tofauti na lile la awali. Ilidhihirika kuwa ugeuzi hufuata utaratibu wa aina maalum. Haufanywi au haufanyiki kiholela. Unatawaliwa na kanuni maalum. Mojawapo wa kanuni zinazoongoza ugeuzaji ni uhusika wa kategoria za kileksia katika tungo, kwa mfano vitenzi vinaweza kuwa na uhusika wa kuelekeza ilhali nomino ikawa na uhusika wa kubainisha mtenda. Kanuni zinazotawala uhamisho vilevile zilishughulikiwa. Baadhi ya hizo kanuni ni kanuni ya ufungami, kanuni hamishe, kanuni ya uhamisho kwa masafa mafupi, kanuni theta na kanuni ya ulafi. Utafiti huu ulibainisha kuwa mchakato wa mageuzi hufanywa kwa kufuata kanuni mahsusi ambazo huitwa kanuni geuzi. Sarufi geuza maumbo inatumia kanuni za aina tatu katika kufanikisha ugeuzi. Sheria hizi ni:

a) Kanuni muundo virai vya sentensi
b) Kanuni geuzi
c) Kanuni za mofofonemiki ambazo huonyesha vipengele vya mwisho vya mofimu.

Utafiti wetu ulidhihirisha kuwa kanuni geuzi zinaweza kusababisha mabadiliko yafuatayo katika sentensi:

i. Huhamisha viambajengo katika sentensi na hivyo kubadili mpangilio wake
ii. Huongeza viambajengo katika sentensi
iii. Hudondosha baadhi ya viambajengo katika sentensi.
iv. Huruhusu uchopekaji wa viambajengo katika tungo.

Geuzi lililojitokeza wazi katika utafiti wetu ni geuzi tendwi na geuzi hamishi. Geuzi tendwi hufanya kazi ya kuigeuza sentensi tendi na kuifanya kuwa tendwi. Geuzi hamishi nalo huathiri mpangilio wa viambajengo katika sentensi. Sifa za kisintaksia zilizodhihirishwa na utendwi na uhamisho kwa mujibu wa utafiti huu ni:

a) Kitenzi kuathirika kimofolojia.
b) Kirai kuwa na dhima ya uhusika.
c) Uhamishi wa kirai nomino kuwa wa kishuruti.
d) Uhamishaji wa kirai nomino kukubalika kwa kuwa nafasi ya kiima ilikuwa wazi.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

Muundo wa sentensi unahusu mpangilio wa viambajengo katika sentensi. Muundo wa virai ya sentensi sahili ya Ekegusii unategemea majopo ya maneno kisarufi. Majopo ya maneno yaliyotumika katika utafiti huuyanaweza kuainishwa katika makundi wawili: Jopo la leksia na jopo amilifu. Kuna categoria tano za maneno zilizoainishwa katika jopo leksia nazo ni nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi na kihusishi. Jopo amilifu hutawaliwa na virai vibainishi, virai vipatanishi na virai shamirisho.

Mchakato hufanywa kwa kufuata kanuni mahsusi zinazoitwa kanuni geuzi. Ugeuzi unafuata utaratibu maalum, haufanywi kiholela. Katika ugeuzi wa maumbo kuna sharti la ukaribu ambapo hakuna kiambajengo kinaweza kuhamishwa zaidi ya fundo funge mbili kutokana na matokeo ya utafiti huu. Kanuni zingine za uhamisho ni kanuni ya ufungami ambapo muundo wa kijenzi kilichofundwa unahitaji uamuliwe na neno tawala linalofaa. Kuna vilele kanuni ya ulafi, kanuni teta na kanuni hamishe. Mwisho kuna kanuni muundo virai, kanuni geuzi na kanuni za mofofonemiki.

Kanuni geuzi husababisha athari mahsusi katika sentensi kimuundo, kimofolojia na kifonetiki lakini kisemantiki sentensi huwa ni ile ile. Nadharia za Sintaksia Finyizi pamoja na nadharia Sarufi Geuza Maumbo ziliweza kuchanganua sentensi za Ekegusii kwa ukamilifu. Athari za mageuzi kwa maneno ya sentensi sahili ya Ekegusii ni pamoja na uhamishaji wa maumbo, uchopekaji wa maumbo na udondoshaji wa maumbo.

Kazi hii imejikita katika uchanganuzi wa athari ya mageuzi ya maneno kwenye muundo wa sentensi sahili ya Ekegusii. Sentensi iliyoshughulikiwa ni sentensi sahili. Kutoka na utafiti huu mtafiti anapendekeza kuwa tafiti zaidi zinaweza kufanywa kuhusu sentensi ambatano au changamano. Isitoshe, utafiti wa mageuzi unaweza kufanywa kwa lugha nyingine ili kueleza iwapo kuna matokeo tofauti. Aina ya geuzi lililoshughulikiwa hapa ni geuzi tendwi na geuzi hamishi. Utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu aina zingine za mageuzi kama vile, geuzi hamishi swalifu, geuzi hamishi la yambwa tendewa katika lugha hii na hata lugha nyinginezo ili kukuza uwanja wa kisintaksia. Kuna uhamisho unaotokea kwa lugha zingine na siyo katika Ekegusii. Hizi pia zinaweza kufanyiwa utafiti. Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni zile za Sintaksia Finyizi na Sarufi Geuza Maumbo. Tafiti zaidi zinaweza kufanyiwa mada hii kwa kutumia nadharia zingine ili kueleza ikiwa kutakuwa na matokeo tofauti. Utafiti huu umedhihirisha kuwa mageuzi ya maneno huongozwa na kanuni mahsusi bali hautokei kiholela.

**MAREJELEO**


Ambuyo, B. A. (2008). *Uamilishi Dhima katika Sentensi za Luloogoli: Mtazamo wa Sintaksia Finyizi*. Tasnifu ya M.A iliyochapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Basweti, N.O. (2005). *A Morphsyntactic Analysis of Agreement in Ekegusii in the Minimalism*

*Programme*.Tasnifu ya M.A ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Brickman, L. & Debra J. R. (2009). *Applied Social Research*. London: Sage Publications.

Bornstein, D. (1978). *An Introduction to Transformational Grammar*. Cambridge: Winthrop Publishers.

Chomsky, N. (1957). *Syntactic Structures*. The Hague: Mouton.

Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge: Massachuessette Institute of Technology Press.

Chomsky, N. (1986). *Barriers*. Cambridge: Massachuessette Institute of Technology Press.

Chomsky, N. (1993). "*A Minimalist Program for Linguistic Theory"* in K. Hale S. J. Keyser (Eds). *The view from building 20 essays in Linguistics in honour of Sylvai Brombergers.* Cambridge: Massachuessette Institute of Technology Press.

Chomsky, N. (1995). *The Minimalist Programme***.** Cambridge: Massachuessette Institute of Technology Press.

Gesare, T. (1992). *Mofolojia ya Lugha ya Ekegusii*. Tasnifu ya M.A iliyochapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Guthrie, M. (1948) .*Classification of Bantu languages*. Oxford: Oxford University Press.

Guthrie, M. (1971). *Comparative Bantu: An Introduction to the Comparative Linguistics Pre-history of the Bantu Language*. Vol 2. Farnborough: Gregy Press.

Habwe, J. H & P. Karanja (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Hendrick, T. E., Bickman, L. & Rog, D.J. (1993): *Applied Research Design.* A Practical Guide. Newburg Park, CA: Sage.

Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Kawa, A. N. (2003). *The Syntax of Noun Movement in Kiswahili*. Tasnifu ya M.A iliyochapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kagwa, F.M., Kombo, K., Waihiga, G. (2013). *Kioo cha K.C.S.E. Kiswahili*. Nairobi: Spotlight Publishers (EA) Limited.

Kapiyo, J., Kiruthu, F., Muma, M. (1996). *The Evolving World. A History and Government course Form 1*. Nairobi: Oxford University Press.

King'ori, A. (2005). *Movement in Kiswahili Sentences: A Minimalist Approach*. Tasnifu ya M.A ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Massamba, D. P. B., Kihore Y. M., Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam; TUKI.

Massamba, D. P. B., Kihore Y. M., Hokororo, J. I. (2004). *Kamusi ya Falsafa na Isimu*. Dar es Salaam: TUKI.

Matinde, R.S. (2012). *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Mayaka, R. O. (2000). *Muundo wa Sentensi ya Ekegusii*. Tasnifu ya M.A ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mbaabu, I. (1992). *Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Longman Kenya.

Mose, L. K. (2013). *Dhima ya Kirai Nomino katika Sentensi ya Ekegusii*. Tasnifu ya M.A. ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mugenda, A. G. (2008). *Social Science Research: Theory and Principles*. Nairobi: ARTS Press.

Nurse, D. & Philipson, G. (1980). *The Bantu Languages*. London: Routledge

Ombuna, O. V. (2014). *Valensi ya Kitenzi katika Kishazi cha Kiswahili.* Tasnifu ya M.A. iliyochapishwa, Chuo Kikuu cha Kenyatta

Otiso, Z. K. (2008). *A Morphosyntactic Analysis of Ekegusii Verb Derivation in Minimalist Programme.* Tasnifu ya M.A. ambayo haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Omondi, L. N. (1992). *Linguistics* (Part III). Nairobi: Nairobi University Press.

Poole, G. (2002). *Syntatic Theory*. Hampshire: Palgrave.

Radford, A. (1997). *Syntax: A Minimalist Introduction*. Cambridge: M.T.I Press.

Thiong'o, N. (1986). *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. London. J. Currey.

Flick, U. (2010).*Introduction to Qualitative Research*. London, UK: Sage Publications Limited.